**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO**
**FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**

Shule ya Sekondari Dkt. Samia Suluhu Hassan,

S.L.P 55,

**NAMTUMBO**

18/04/2024

Mkuu wa Shule: 0755083649/0654988030
Mwalimu Elinikunda W.Lema: 0764650332
Kumb.Na DSSHS/E./

Bi…………………………………………………….....

……………………………………………………………

……………………………………………………………

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KWA KIDATO CHA TANO.

1. Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii. Jumuiya ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Dkt. Samia Suluhu Hassan.

(**DKT. SAMIA SULUHU HASSAN SECONDARY SCHOOL)** inasema HONGERA NA KARIBU SANA. Ni mategemeo yetu utafurahia maisha kwa muda wote utakaosoma hapa na kwamba utaonyesha tabia njema, utakuwa na ari ya kujifunza na utajitahidi,kutekeleza shughuli zote zinazomhusu mwanafunzi kwa juhudi na maarifa.Walimu, Wafanyakazi, Wanafunzi wenzakona wanajumuiya wote kwa ujumla wapo tayari kukupa kila msaada utakaohitaji pale itakapolazimika.

Shule ya Sekondari Dkt. Samia suluhu Hassan iko umbali wa kilomita saba (7) kutoka stendi kuu ya mabasi ya Namtumbo Mashariki mwa Halmashauri ya wilaya Namtumbo, ikiwa jirani na hospitali mpya iliyopo migelegele barabara ya SONGEA-MTWARA. Ili uweze kufika shuleni kwa urahisi, kwa wanaotoka nje ya Mkoa wa Ruvuma, panda basi la Super Feo au Selous Express, SHUKA KITUO STENDI YA MABASI **NAMTUMBO,**aidha Kutoka Songea mjini unapanda gari za Namtumbo stendi ya **SEEDFARM**,umbali kutoka stendi ya seedfarm mpaka Namtumbo ni kilometa 68. Kuna usafiri wa bajaji na pikipiki **kutoka stendi ya N amtumbo hadi shuleni, hakikisha umechukua Fomu ya Maelekezo ya Kujiunga na Shule (Joining Instructions), itakayokutambulisha kama mwanafunzi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kondakta/dereva wa mabasi hayo ambapo**

**watakusaidia namna ya kufika shuleni salama.(Tafadhali zingatia maelekezo haya). UNATAKIWA KURIPOTI SHULENI TAREHE ITAKAYOTANGAZWA NA WIZARA KWA MUHULA WA KWANZA WA MASOMO**. Unatakiwa kufika Shuleni tarehe husika. Mwanafunzi atakayechelewa kuripoti pasi na taarifa ya kuchelewa kwake atakuwa amepoteza nafasi hii.

**Tafadhali kama umepata shule sehemu nyingine na hutaripoti, toa taarifa shule hapa kwa barua ili wizara ifanye utaratibu wa kumpa nafasi mwingine mwanafunzi mwingine , aidha baada ya miezi mitatu toka tarehe ya kuripoti shule, kama utakuwa hujafika shuleni basi wizara itafanaya utaratibu wa kujaza nafasi hiyo nawe utakuwa umepoteza nafasi hiyo.**

**Mambo muhimu ya kuzingatia:-Sare ya shule**

Mwanafunzi aje na sketi mbili za Draft (Sample ya kitambaa imeambatanishwa). Sketi zake ziwendefu kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi zisizidi sentimeta 18 au inchi 7 ½. (**Kama huelewi juu ya upatikanaji wa kitambaa njoo n ash.35000/ utashonea shuleni sketi 2)**

- Sketi zake zisiwe na (belt) mkanda mpana, upana wa belt usizidi sentimeta 05 au inchi moja na nusu.
- Tai ndefu rangi ya sketi (draft) yenye alama ya V nyeupe.
- Marinda – pembeni pande zote mbele na nyuma marinda madogo matatu, katikati rinda box moja au rinda pana moja. Sketi isibane iwe na upana wa kutosha. Mchoro wa mshono wa sketi umeambatanishwa na barua hii.
- Sketi zake ziwe ndefu sana, na siyo fupi zingatia urefu wa sentimeta 18 au inchi 7 ½ kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi.
- Mzazi/mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo hivyo, mwanafunzi atakayeshona na kuja na sketi/shamba dress kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichoelekeza hatapokelewa, atarudishwa nyumbani ili aje na sare zilizoelekezwa.
    - Mchoro wa mshono wa gauni umeambatanishwa.
    - Mwanafunzi aweke alama ya jina lake na la mzazi wake kwenye sare na vitu vyake vyote kuepuka kuibiwa/kupotea.

**2. Mwanafunzi anapaswa kununua sare zifuatazo:-**

(i) Shati (blauzi) nyeupe mbili (2) au zaidi mikono mifupi tetroni – Tomato

(ii) Kiatu -Juma na Roza (ZISIWE NA KISIGINO KIREFU; high heels) jozi mbili (02) au zaidi (mfano wa kiatu umeoneshwa hapo chini)

(iii) Soksi nyeupe jozi mbili (2) au zaidi.

(iv) Aje na barakoa angalau 4 zinazofuliwa na kupigwa pasi (cotton) (sawa na rangia ya sketi).

(v) Kwa wanafunzi wa Kiislamu: Vazi la Msikitini
- Suruali bluu ya heshima na isibane
- Blauzi bluu ndefu ipite magoti na yenye mikono mirefu.

- Hijabu ya tetroni nyeupe/juba na sio mtandio, isiwe na urembo wowote. Pia isiwe na urembo wa lessi.

(vi) Bukta nyeusi kwa ajili ya michezo iwe ndefu ifunike magoti.
(vii) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo
(viii) T-shirt ya michezo **TAIFA STARS NYEUPE**.
(ix) Truck Suit light blue (Adidas) isiyobana kwa ajili ya maandalizi yajioni.
**(x)** Aje na T-Shirt ya Shule dark blue moja **(Kama huelewi juu ya upatikanaji wa T-SHIRT DARK BLUE, njoo na sh.15,000/= utaipata shuleni)**

- Aje na sweta la damu ya mzee, shingo ya V.

Mwanafunzi anaweza kushona idadi ya sare kadiri ya uwezo wake. Ila inashauriwa awe na angalau sare za darasani mbili na gauni za kazi mbili.

**Kwa wale watakaokuja kushonea shuleni, waje wakiwa wamevaa track suit ya shule na sio nguo za nyumbani. Huruhusiwi kabisa kuja na nguo yoyote ya nyumbani kama vile kikoi, mtandio n.k.**

Sare ya shule ni kama ilivyoelekezwa katika maelekezo. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare wakati wote wa masomo, na anapokwenda hospitali, mjini au anapokuwa katika shughuli zozote za kishule nje ya eneo la shule. Ni marufuku kabisa kujipamba wakati amevaa sare ya shule akiwa shuleni. Aidha, lipo vazi la kazi za nje ambalo huvaliwa na wanafunzi wanapokuwa katika kazi za mikono nje yama somo.

### 3. Mahitaji Mengine Muhimu kwa Mwanafunzi.

i. Awe na sanduku (nunua sanduku la bati) linalofunga vizuri kwa kuhifadhia nguo na vitu vyake.
ii. Aje na godoro la ukubwa wa futi 2 ½ kwa futi 6.
iii. Aje na Mto na Foronya yake
iv. Blanket moja la futi 2 ½ x 6
v. Aje na bed cover (shuka moja) ya BLUU BAHARI futi 2 ½ x 6 na foronya ya pinkvisivyo na maua au urembo wowote.
vi. Shuka za Kulalia mbili za futi 2 ½ x 6 (rangi ya BLUU BAHARI)
vii. Taulo moja (01) au mbili (02)
viii. Koti la mvua au mwavuli
ix. Kandambili kwa ajili ya kuogea.
x. Viatu vya plastiki chipsi (BAJAJI) rangi yoyote – vya kushindia.
xi. Aje na kifaa kimoja (01) kulingana na mkondo wake, kama ilivyohainishwa hapo chini:

HGK –Reki
HGL – Kwanja
PCB-Ndoo kubwa
CBG – Panga
HKL – Fagio refu la kutolea buibui.

**Vifaa vifuatavyo vitaletwa na wanafunzi wote**

xii. Soft broom moja (01).

xiii. Hard broom moja (01)

xiv Squeezer kwa ajili ya kudekia/kukaushia maji sakafuni. (mopa)

xvi. Ndoo ndogo mbili (moja kwa matumizi ya shule na nyingine kwa matumizi yake binafsi bwenini).

xvii. Fagio la chelewa mbili (02) kwa muhula, nne (04) kwa mwaka.

xviii. Jembe moja na mpini wake.

xix. Alete container lenye mfuniko/sahani, bakuli, kikombe na kijiko. (Pia vinapatikana kwenye duka la shule)

xx. Daftari (counter books) quire three zisizopungua kumi (10) kwa ajili yakutunzia notes. (Pia vinapatikana kwenye duka la shule)

xxi. Daftari nyingine aina yoyote kwa ajili ya mazoezi kwa kila somo.

xxii. T- shirt yenye rangi ya kijivu kwa ajili ya michezo.

xxiv. Graph pad nne (04) kwa mwaka, isipokuwa wanaosoma HKL.

xxv. Ream moja ya karatasi A4 (photocopy paper) kila muhula, rimu 2 kwa mwaka

xxvi. Jalada/faili moja au mbili kwa kujitunzia nyaraka zake za kitaaluma (matumizi yake binafsi)

xxvii. Mathematical set moja (01) kwa matumizi yake awapo darasani. Isipokuwa HKL, wao wasilete.

xxviii. Kwa wanafunzi watakaosoma BAM au ADVANCED MATHEMATICS ni vizuri wanunue Scientific Calculator fx 991

**MICHANGO MBALIMBALI**

xxix. Mchango wa uendeshaji wa shule 65,000/=

xxx. Tahadhari 5,000/=

xxxi. Nembo 5,000/=

xxxii. Kitambulisho cha shule 5,000/=

**Jumla 80,000/=**

**Akaunti No.0150742874700 CRDB** (Dkt.Samia Suluhu Hassan sec. school) na mwanafunzi afike na risiti ya kutumia fedha Benki.**Tafadhali nasisitiza hatutapokea fedha mkononi.**

xxxiii. Alete chandarua nyeupe/blue ya kitanda cha futi 2 ½ x 6.

xxxiv. Dissecting kit (kwa wanaosoma Biology).

xxxv. Koti la maabara jeupe (wanaosoma Sayansi, CBG na PCB).

xxxvi. Alete Tsh. 50,400/= kwa ajili ya bima ya afya kwa mwaka (kwa wale ambao hawana Bima ya Afya, Aje pia na Kadi ya NIDA au NAMBA YA NIDA kwa aliyefikisha umri wa miaka 18). Ni muhimu sana kwani itamsaidia kutibiwa kwa mwaka

mzima sehemu yoyote nchini.

(Fedha hii sio sehemu ya mchango wa shule, hivyo alete fedha taslimu. Asiingize kwenye akaunti ya shule)

Orodha ya vitabu vinavyotakiwa kwa masomo imeambatanishwa, mzazi/mlezi mwenye uwezo unaweza kumnunulia mwanao aje navitabu hivyo kulingana na masomo/tahasusi husika kulingana na uwezo wako.

## Fedha za tahadhari (Caution Money)

Kila mwanafunzi atatoa Tsh.5,000/= za tahadhari. Endapo utapoteza au utaharibu kitu ambacho ni mali ya shule, tutakata fedha hizo. Kama thamani ya kitu ulichoharibu/kupoteza ni zaidi ya Tsh. 5,000/= utadaiwa fedha nyingine zaidi. Fedha hizi hazitarudishwa umalizapo shule kwani zitasaidia kukarabati vifaa ambavyo utakuwa umevitumia miaka miwili (tear and wear).

### 4. Fedha za Matumizi

Mzazi anashauriwa akupatie fedha za kutosha kwa matumizi yako binafsi. Kuna duka la shule ambalo huwapatia wanafunzi mahitaji yao muhimu. Aidha, mwanafunzi haruhusiwi kuweka fedhaBwenini, mkabidhi Mhasibu akutunzie. Vilevile Mzazi/Mlezi atume fedha ya matumizi ya mwanafunzi kwa kupitia namba ya shule ambayo itatolewa au 0755083649/0654988030 **Mkuu wa Shule,** pia namba za Ofisi ya Malezi Elinikunda W.Lema: 0764650332, Mzazi ukitumia fedha line ya shule andika ujumbe kumtambulisha mhusika, Mfano; Nimetuma shilingi 30,000/= kwa mwanafunzi Veronica James kidato cha tano PCB. Aidha, Mwanfunzi hatapata ruhusa ya kwenda kufuatilia fedha sehemu nyingine. Mfano kwa ndugu nje ya shule, Benki, n.k

**NB:** Hii ni kwa fedha za matumizi tu.

### 5. Chakula

Shule hutoa chakula ambacho huliwa na Watanzania wote, ambacho Serikali inapendekeza kuliwa na mwanafunzi. Endapo unayo miiko ya kutokula vyakulafulani, tafadhali usipokee nafasi hii kwani shule haitatoa huduma ya pekee kwa kila mwanafunzi. Pia shule haitoi kibali kwa mwanafunzi kujipikia hivyo asilete chakula kama mchele, unga, biskuti, mkate, kinywaji cha aina yoyote n.k. na haturuhusu mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula/kinywaji toka nje ya shule.

### 6. Tahadhari

Fedha kwa ajili ya michango yote aliyoagizwa na shule iingizwe kwenye **akaunti ya Shule No. 0150742874700 Benki ya CRDB (SHULE YA SEKONDARI DKT SAMIA SULUHU HASSAN)** ajapo shuleni awasilishe Benki Pay in Slip aliyotumia fedha hizo. Fedha Taslimu haitapokelewa.

## 7. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Mwanafunzi ni lazima akumbuke kuwa, ni marufuku sare ya shule kuvaliwapamoja na vitu vifuatavyo:

a. Kofia
b. Hereni
c. Bangili
d. Viatu vya ghorofa (high heels)
e. Pete, Mkufu, Shanga n.k.
f. Vibanio vya nywele n.k.
g. Kupaka wanja, rangi ya midomo.

## TAALUMA

Mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya masomo na kufanya mazoezi yote anayopewa na mwalimu wa somo husika. Asipofanya hivyo atapewa adhabu ikiwemo kurudishwa nyumbani.

Kila mwanafunzi anatakiwa apate alama zisizopungua $\frac{50}{100}$ kwa kila somo analosoma kwenye mitihani yote. Akishindwa kufikisha alama hizo kwa somolololote hataruhusiwa kwenda likizo.

Mwanafunzi alete matokeo yake ya kidato cha nne (result slip) na cheti cha kuzaliwa.

**8. Mwanafunzi anatakiwa awe na nywele fupi - Njiti ya kiberiti ikichomekwa kwenye nywele ionekane. Haruhusiwi kusuka nywele.**

**9. Yafuatayo ni makosa ambayo baada ya kuthibitishwa yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule mara moja:-**

a. Wizi
b. Uasherati na Ushoga
c. Ulevi wa aina yeyote
d. Uvutaji wa Bangi na madawa mengine ya kulevya
e. Makosa ya jinai
f. Kupigana
g. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
h. Kuolewa
i. Kudharau Bendera ya Taifa au Wimbo wa Taifa
j. Kuwa na mimba/Kutoa mimba
k. Kukataa adhabu kwa makusudi
l. Kugoma, Kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama washule na watu.
m. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi na kifaa chochote kinachohusiana na simu, Radio, TV Camera, Kisu n.k.
n. Utoro au kutoka nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule.
o. Kumiliki silaha ya aina yoyote.
p. Kumiliki camera ya aina yoyote.
q. Kumiliki kipasha joto (heater).

**N.B: Tafadhali mshauri mwanao azingatie/afuate maelekezo yote aliyopewa! Akipatikana na kosa litakalosababisha arudishwe nyumbani, atajigharamia nauli ya kwenda na kurudi**.

## Sheria za Shule

Mwanafunzi anapaswa kufuata kikamilifu sheria na taratibu zashule kama zilivyoelekezwa. Mfano:-

Kutotumia lugha mbaya kwa walezi au kwa wanafunzi wenzake Kutochelewa kuripoti mara shule inapofunguliwa

Kutohudhuria vipindi ndani na nje au kushindwa kuhudhuria mandalio yamasomo (Preparation).

Kuhudhuria mahali anapotakiwa awepo kwa wakati stahiki.Taratibu nasheria nyingine za shule atasomewa mara baada ya kufika shule.

## NGUO NYINGINE

Aje na khanga au kitenge doti moja au zaidi. Aje na nguo za ndani za kutosha Mwanafunzi atakayeshona sare nyumbani aje akiwa amevaa sare za shule. Mwanafunzi anaruhusiwa kuvaa Track Suit wakati wa maandalio ya jioni ili kujizuia na mbu. Kinyume na hapo atarudishwa nyumbani kurejesha nguo zisizotakiwa kwa gharama zake.

Masanduku/mabegi makubwa hayaruhusiwi, kwani hatuna nafasi ya kuyatunza. Akija nalo atalazimika kurudisha kwa gharama zake.

## 10. ANGALIZO KWA MZAZI/MLEZI

(i) Shule inafuata mihula inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, hivyo inakuwa na mihula mirefu miwili na mifupi miwili kwa mwaka. Mzazi /mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto anawasili kwa wakati shuleni, vinginevyo sheria itachukua mkondo wake.

(ii) Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia Mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule na ofisi ya Malezi. Mwanafunzi **haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi awapo shuleni**.

(iii) Shule haina utaratibu wa kuwaona wanafunzi isipokuwa mzazi ataitwa na uongozi wa shulekama kuna ulazima wa kufanya hivyo.

(iv) Aidha unashauriwa kutomruhusu mwanao kumiliki simu kipindi hiki ambacho umri wake unampa shida kuyatawala mazingira ya utandawazi.

(v) Mzazi/mlezi kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apotezeutulivu wa maisha ya shule na kuvunja sheria za shule.

(vi) Shule ina utaratibu wa kushughulikia usafiri kwa wanafunzi wanaotoka mbali kipindi shule inapofunga. Hivyo mzazi/mlezi utapewa taarifa kabla ya shule kufunga.

(vii) Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.

**(viii) Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara, tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na akabidhi kwa MuuguziMatron wa Shule. Hii itarahisishia shule kumhudumia. Usipofanya hivyo shule itashindwa kumhudumia. Usifiche ugonjwa,**

**utapokelewa tu, kupata elimu ni haki yako.**

(ix) Mwanafunzi anaruhusiwa kuleta pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo zake. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na kutumia pasi ya umeme ama kifaa chochote kinachotumia umeme. Akibainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa shule.

(x) Shule itakapokuwa imefunga, likizo zote **mwanafunzi atatokea shuleni moja kwa moja kwenda kwa mzazi wake (nyumbani kwao) na shule itakapofungua atatokea nyumbani kwao (kwa mzazi) moja kwa moja kuja shuleni**. Atakayekiuka utaratibu huu atarudishwanyumbani kwa gharama zake.

**(xi)** Mwanafunzi haruhusiwi kuja na kumiliki simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu, hata kama anatoka mbali. **AKIJA NAVYO ATAFUKUZWA SHULE (ATAFUTWA SHULE MARA MOJA).**

11. MKUTANO WA WAZAZI/WALEZI

Kutakuwa na mkutano/ kikao na wazazi/walezi angalau mara moja kwa mwaka. Tarehe ya mkutano wazazi watajulishwa. Unaombwa kuhudhuria upatapo nafasi,kwa maendeleo ya shule.

**12. Pamoja na barua hii, Pokea**

(a) Fomu ya kupimwa afya yako. Upimwe kwenye Hospitali ya Serikali. Hakikisha unapimwa sio kujaziwa fomu tu, na umweleze Mganga matatizo ya afya uliyonayo, kwani hatutapokea hoja zozote za ugonjwa kinyume na ripoti ya daktari.

(b) Fomu ya kuonyesha ndugu wa karibu na eneo la shule ikiwa na anuani, namba ya simu na sehemu anakoishi pamoja na ahadi ya kutekeleza wajibu. Picha za walezi/ndugu wa karibu ziambatanishwe kwenye fomu hiyo pamoja na kugongwa muhuri na Mtendaji wa mtaa/kijiji.

Kwa kumalizia, nakutakia maandalizi mema na safari njema kuja kujiunganasi. Utakapofika daima kumbuka kuwa msimamo wa shule hii ni kauli mbiu (MOTTO) ni KUMJENGEA UWEZO MTOTO WA KIKE KUUBADILI ULIMWENGU. **(INSPIRE GIRLS FOR CHANGE)**

(c) Mzazi/mlezi ni lazima uandike Sanduku la Posta.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

DAFROSA C. CHILUMBA

**MKUU WA SHULE**

THE HEADMISTRESS
DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 55
NAMTUMBO

## MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

Dkt. Samia Suluhu Hassan Secondary School

P.O BOX 55

**NAMTUMBO**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Please examine Miss
.......................................................................... as her physical andmental fitness for admission as a form ...................................................Students at Dkt. Samia Suluhu Hassan Secondary School in the year ..................

Your sincerely.

DAFROSA C. CHILUMBA
**The headmistress,**

THE HEADMISTRESS
DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
SECONDARY SCHOOL
P.O BOX 55
NAMTUMBO

The headmistress,
I have examined Miss ............................................................................ as shown and consider that she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full-time secondary schooleducation.

1. Vision with/without glasses. Right ........................... Left ...........................
2. Blood pressure ................................ Hemoglobin ...........................
3. Hearing ....................................................................................
4. Urine (a) Albumen.............................. (b) ...............................................
5. a)Venereal diseases.............................. (b)Bilharzia..............................
6. Pregnancy ....................................................................................
7. Neurosis....................................................................................
8. Is there any abnormality of :
   a) The heart.................................. b) Lungs ........................
   c) The spleen ........................................
9. Are there serious diseases. E.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma, Diabetes, etc.
   ........................................................................................ Date
   .............................. Signature of the medical Officer ........................ Station
   ..................... Designation ...................................

## SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN.

**FOMU MAALUM INAYOONYESHA TAARIFA ZA NDUGU WA JIRANI NAMWANAFUNZI**

Ndugu wa karibu na mwanafunzi: Hakikisha unaandika majina mawili na anwani zao.Hii inasaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo litatokea . Hatutaki majina ya ndugu wa bandia.

1. (a) Jina :_______________________________________________
   (b) Uhusiano: ________________________________________________
   (c) Anwani:__________________________________________________
   (d) Namba ya Simu:__________________________________________

Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji___________________________________Muhuri

Namba ya simu ..............................

2. (a) Jina :_______________________________________________
   (b) Uhusiano: ________________________________________________
   (c) Anwani:__________________________________________________
   (d) Namba ya Simu:__________________________________________

Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji_________________________________Muhuri

Namba ya simu ..............................

Saini ya mzazi: ___________________________

Tarehe: _____________________________

**YAH: AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU**

Mimi____________________________________________nakubali nafasi niliyoipata katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuendelea na masomo yangu. Nafahamu ninagharamiwa na Taifa linadhamini kazi na juhudi. Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitajitahidi upeo wauwezo wangu kuwa mwanafunzi mwema. Naahidi nitashirikiana na Walimu, Wafanyakazi wasio walimu pamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa Shule na Taifa kwa ujumla.

_________________

Saini ya mwanafunzi

Mimi_______________________________________nimesoma yote na kuelewa . Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua, ripoti na taarifa zote zinazomhusu Binti yangu kwa anwani ifuatayo:

_____________________________________


__________________________________________

Jina na saini ya mzazi/mlezi: ____________________________________________

Tarehe:___________________________________Namba ya simu ______________________

## 1. SKETI ZA DARASANI (ZIWE MBILI)

**NB: Mchoro huu hapa chini unaonyesha namna ya mshono**





**kitambaa**



**2. GAUNI (SHAMBA DRESS) ZA KUSHINDIA- ZIWE MBILI**

- Iwe mshono wa solo kama ilivyo katika mchoro.
- Kitambaa rangi dark bluu.
- Kifuani ziwe na upana wa kutosha, isibane
- Urefu toka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la gauni usizidi sentimeta 18 auinchi 7½.



**ORODHA YA VITABU**


**1. HISTORY**

- Edward John (2011), **Advanced Learners History Form 5 and 6**. Oxford University Press (T) LTD.
- Shibitali & Tumaini (2011) **Recent Historical Surveys**. Dar es Salaam, Shibitali & Sons Publishers. (1&2).
- Mastering of History Book One and Two, Advanced Learners History for Form 5 and 6.
- Saleh Yassin, **Essentials in Advanced Level History Paper 1 & 2**. Ahmadiyya Printing Press.
- Mwl. Kato A.K **Mastering Advanced Level History**. Mweas Book Publishers and Suppliers Mwanza Tanzania.

**2. PHYSICS**

- **Advanced Level Physics, 7th Edition** by Nelkon and Parker.
- S. Chand's **Principles of Physics for Class XI** by V.K Mehta & Rohit Mehta.
- S. Chand's **Principles of Physics for Class XII** by V.K Mehta & Rohit Mehta.
- **A Level Physics, 4th Edition** by Roger Muncaster.
- **Advanced Physics, 5th Edition** by Tom Duncan.
- **Fundamentals of Physics, 5th Edition**, by Halliday Resnick Walker.
- **Electronics for Today and Tomorrow, 2nd Edition** by Tom Duncan.

**3. CHEMISTRY**

- S.K SAIN (2016) **Conceptual Chemistry for Class XI and XII**, S. Chand School Books.
- A. Bahl, B.S. Bahl & G.D Tuli (2012) **Essential of Physical Chemistry**, S.Chand & Company Pvt. Ltd.
- N.K. VERMA, S.K KHANNA & B. KAPILA (2012**) Comprehesive Chemistry Volume I & II for Class XII** , Laxmi Publication (P) Ltd Golden Home New Delhi.
- G.D Tuli & R.D MADAN (2011) **Advanced Inorganic Chemistry**, S. Chand & Company Ltd.

**4. BIOLOGY**

- Taylor (D.J), **Biological Science 3rd Edition**
- Glenn G et al (1999), **New Understanding Biology For Advanced Level, 4th Edition**, Oxford University Press.

**5. GEOGRAPHY**

- **Physical Geography in Diagrams For Africa** (R.B. Bunnett).
- **Practical Geography for Africa** (John M. Pritchard).
- **Physical Geography** (D.T. Msabila).
- **Human and Economic Geography** (G.C. Morgan).
- **Geography An Integrated Approach** (David Waugh).
- **Principles of Physical Geography** (F.J. Monkhouse)
- **Atlas**
- **Lanforms in Africa** (Collin Buckle)
- **General Geography** (R.B. Bunnet)

6. **GENERAL STUDIES**

- **Understanding General Studies for Advanced Level** by Joannes Bigirwamungu and Sospeter M. Deogratias.
- **General Studies for Advanced Level Certificate Form Five and Six** by Richard R.F Mbalase.

7. **ECONOMICS**

- Dr H.L. Ahuja (2008**), Principles of Microeconomics 20th Revised Edition** S. Chand & Company Ltd.
- Dr H.L. Ahuja (2019), **Advanced Economic Theory**, Chand & Company Ltd.
- Dr K.K. Dewett (2015), **Modern Economic Theory Revised Edition**, S. Chand Publishing.
- Ddumba Ssentamu J (2004), **Basic Economic for East Africa 1st Edition** Fontain Publishers, Kampala Uganda.
- Tayebwa B.M. Bernard (2011) **Basic Economics, 5th Edition**, Genuine Publishers and Consultants Ltd.

8. **ADVANCED MATHEMATICS**

- Septine I. Sillem (2015), **Advanced Mathematics for Secondary School Form V**, Gdy Publisher.
- Septine I. Sillem (2015), **Advanced Mathematics for Secondary School Form VI**, Gdy Publisher.
- Clement John Tranter (1975), **'Advanced Level Pure Mathematics'** Hodder & Stoughton, United Kingdom.
- J.K. Backhouse (1985), **'Pure Mathematics 1'** S.P.T Houldsworth et al.
- J.K. Backhouse (1985), **'Pure Mathematics 2'** S.P.T Houldsworth et al.
- J Crawshaw & J. Chambers (1994), **A CONCISE COURSE IN A – LEVEL STATISTICS**, Stanley Thornes (Publishers) Ltd , The Bath Press Avon Britain
- A.J. Sadler & D.W.S Thorning, '**Understanding Pure mathematics'** Oxford University Press.
- L. Bostock, S. Chandler & C. Rourke**, 'Further Pure Mathematics'** Oxford University Press.
- L. Bostock, S. Chandler**, 'MATHEMATICS The Core Course for A- level'** Oxford University Press.
- H.K DASS & Dr RAMA VERMA (2008), **'MATHEMATICS FOR CLASS XII, VOLUME II'** S. Chand's Publishers.

9. **KISWAHILI**

**(a) RIWAYA**

- Vuta N'kuvute
- Mfadhili
- Usiku Utakapokwisha

**(b) TAMTHILIYA**

- Kivuli Kinaishi.
- Morani.

**(c) USHAIRI**

- Kimbunga
- Chungu Tamu
- Fungate ya Uhuru

**(d) SARUFI**

- Samakisa
- Samikisa
- Kitangulizi cha Tafsiri by Mwansoko.
- Nadharia ya Lugha by Nyangwine.
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu.

**10. ENGLISH LANGUAGE**

**(a) PLAYS**

- Betrayal In the City – Francis Imbuga
- I Will Marry When I Want – Ngugi wa Thong'o and Ngugi wa Mirii.
- The Bride – Austine Bukenya.
- Lwanda Magere – Okoiti Omtatah.
- An Enemy of The People – Henrick Ibsen
- Black Mamba – John Ruganda

**(b) NOVELS**

- Encounters From Africa – Macmillan Education Limited
- The Beautiful Ones Are Not Yet Born – Ayi Kwei Armah
- A Man of The People – Chinua Achebe
- Divine Providence – everin N. Ndunguru
- The Rape of The Pearl – Magala Nyayo
- Vanishing Shadow – Namige Kayondo
- His Excellencey The Head of State – Danny Sato
- A Season of Waiting – David Omowale

**(c) POETRY**

- Selected Poems – Tanzania Institute of Education (TIE)
- The Wonderful Surgeon and Other Poems – Charles MLoka

**OTHER ENGLISH LANGUAGE BOOKS**

- ADVANCED LEVEL ENGLISH, A PRACTICAL APPROACH 2nd EDITION – Nicholous Asheli.
- OXFORD ADVANCED LEVEL DICTIONARY 8th EDITION
- ADVANCED ENGLISH FORM 5 AND 6, 1st EDITION – OXFORD UNIVERSITYPRESS, John J.

- ENGLISH PHONETICS AND PHONOLOGY – Peter Roach.
- ADVANCED LEVEL LITERATURE FORM 5 AND 6 – Godfrey Rulta Bukagile.m